# WASIFU (PROFILE) YA TUME

## KUANZISHWA KWA TUME

Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013 ikiwa ni Idara inayojitegemea chini ya iliyokuwa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Baada ya Serikali kuridhia kuibadili kutoka kuwa Idara ya Maendeleo ya Ushirika. Majukumu makuu ya Tume ni kusimamia na kuhamasisha maendeleo ya Ushirika Tanzania Bara. Kisheria Tume ilianza shughuli zake tarehe 1 Januari 2014, ilipotangazwa kwenye Gazeti la Serikali na Waziri mwenye dhamana ya Ushirika, lakini utekelezaji wa majukumu yake kama yalivyoainishwa kwenye muundo wa Tume ulianza mwezi Februari 2015 baada ya kupitishwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Maelezo ya Kazi (Job Descriptions) na Mahitaji ya Watumishi (Job List) yalipitishwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma mwezi Julai 2015.

Tume ya Mandeleo ya Ushirika Tanzania imepewa mamlaka ya kuwa mwangalizi wa uongozi na utendaji kazi wa Vyama vya Ushirika, ikihakikisha kufuatwa kwa Sheria na Kanuni za Ushirika.

### 1. Dira ya Tume

Dira ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania ni *Kuwa Taasisi mahiri ya udhibiti kwa maendeleo ya Ushirika Tanzania*

### 2. Dhamira ya Tume

Dhamira ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania ni *Kutoa huduma za udhibiti na Uhamasishaji zenye ufanisi na ubora ili kuwa na Ushirika wenye nguvu, bunifu na endelevu kiuchumi.*

### 3. Tunu za Tume (Maadili ya Tume)

- Weledi (Professionalism)
- Ushirikiano (Team Work Spirit)
- Uwajibikaji (Accountability)
- Uwazi (Transparency)
- Uadilifu (Integrity)

- Utendaji unaozingatia matokeo (Results oriented)
- Ubunifu (Innovation and Creativity)
- Kuthamini wateja (Customer oriented)

## 4. Majukumu ya Tume

Katika kutekeleza kazi ya Usimamizi na Udhibiti; Tume ina majukumu yafuatayo:-

- Kuandikisha na kufuta vyama vya Ushirika;
- Kukagua na kusimamia vyama vya Ushirika;
- Kuhifadhi na kuendeleza rejista ya Vyama vya Ushirika;
- Kuhakikisha majina ya Vyama vya Ushirika vilivyoandikishwa na/au kufutwa kwenye Daftari la Usajili wa Vyama vya Ushirika yanatangazwa kwenye Gazeti la Serikali;
- Kudhibiti na kutatua migogoro na malalamiko yanayoibuka katika Vyama vya Ushirika;
- Kushirikiana na mamlaka za TAMISEMI katika kutekeleza kazi ya usimamizi na udhibiti wa shughuli za Vyama vya Ushirika; na
- Kusimamia utekelezwaji wa kazi nyingine za usimamizi na udhibiti kama itakavyotakiwa kwa mujibu wa matakwa ya Sheria.

Pia, katika kutekeleza kazi ya Uhamasishaji, Tume ina majukumu yafuatayo:-

- Kusimamia na kuratibu jukumu la uhamasishaji kwa kushirikisha Wizara za kisekta, Mamlaka za Tawala za Mikao na Serikali za Mitaa na wadau wengine;
- Kuhimiza na kuhamasisha uendelezaji wa Vyama vya Ushirika endelevu na vyenye uhai wa kiuchumi;
- Kuratibu uandaaji wa mipango ya kiuchumi ya Vyama vya Ushirika na utekelezaji wake ili ijumuishwe katika mipango ya maendeleo ya kitaifa;
- Kusaidia kitaalam katika kutekeleza Sera zenye mwelekeo wa maendeleo ya ushirika;
- Kuwezesha kujenga na kuendeleza uhusiano au ushirikiano kati ya wadau wa maendeleo ya ushirika wa ndani na nje ya nchi; na

- Kusimamia na kuratibu jukumu la uhamasishaji kuhusu masoko na uwekezaji kwa kushirikisha wadau mbali mbali, Wizara za kisekta na Serikali za Mitaa.

## 5. Muundo wa Tume

Muundo wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika uliidhinishwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 2015, ambapo Tume inasimamiwa na Kamisheni inayoongozwa na Mwenyekiti ambaye anateuliwa na Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania na Makamishna kumi (10) wanaoteuliwa na Waziri mwenye dhamana ya Ushirika.

Aidha, shughuli za utendaji wa kila siku za Tume zinaongozwa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika nchini na Mtendaji Mkuu wa Tume ambaye ndiye Katibu wa Kamisheni. Mrajis anasaidiwa na Manaibu Warajis wawili (2); wenye dhamana ya Udhibiti na Uhamasishaji wa Maendeleo ya Ushirika mtawalia. Mrajis pamoja na Manaibu wake wanateuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa mujibu wa Muundo ulioidhinishwa, Tume ina Divisheni tatu (3) ambazo ni Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu, Udhibiti pamoja na Uhamasishaji.


Tume ina Vitengo nane (8) ambavyo ni Mipango Ufuatiliaji na Tathmini, Utafiti na Mafunzo, Uhasibu na Fedha, Mawasiliano Serikalini, Huduma za Kisheria, Ununuzi na Ugavi, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, na Ukaguzi wa Ndani.

Vilevile, Tume ina Sehemu saba (7) ambazo ni Sheria na Usajili, Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama Visivyokuwa vya Kifedha, Usimamizi na Udhibiti wa Vyama vya Ushirika wa Kifedha, Uhamasishaji na Uratibu, Masoko na Uwekezaji, Utawala na Rasilimaliwatu.

Tume pia ina Ofisi za Mikoa zinazoongozwa na Warajis Wasaidizi katika Mikoa yote 26 ya Tanzania Bara na Ofisi za Wilaya zinazoongozwa na Maafisa Ushirika wa Wilaya kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za udhibiti na uhamasishaji.

THE FUNCTIONS AND ORGANISATION STRUCTURE OF THE COOPERATIVE DEVELOPMENT COMMISSION

*(Approved by the President on 12th February, 2015)*



## I. Kamisheni ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika

1. Dkt. Abdulmajid Nsekela - Mwenyekiti wa Kamisheni
2. Bi. Irene Madeje Mlola - Makamu wa Mwenyekiti
3. Mhe. Zainab Telack - Mjumbe
4. Prof. Godfrey Nyange - Mjumbe
5. Prof. Alfred S. Sife - Mjumbe
6. Bw. Shaibu Ahmed Nnunduma - Mjumbe
7. Bw. Patrick Stephen Malogoi - Mjumbe
8. Bw. Richard Malulu Mayongela - Mjumbe
9. Bi. Happy Richard Kitingati - Mjumbe
10. Bw. Godfrey Ng'urah - Mjumbe
11. Bw. Paul Kachemba - Mjumbe

## II. Menejimenti ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Dkt. Benson O. Ndiege | Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa TCDC, Katibu wa Kamisheni |
| 2. | Bw. Collins B. Nyakunga | Naibu Mrajis- Usimamizi na Udhibiti |
| 3. | Bi. Consolata J. Kiluma | Kaimu Naibu Mrajis – Uhamasishaji |
| 4. | Bw. Gabriel Mwitta | Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimaliwatu |
| 5. | Bi. Flora P. Bilauri | Mkurugenzi wa Mipango, Tathmini na Ufuatiliaji |
| 6. | Bw. Juma Mokili Juma | Mkurugenzi wa Utafiti na Mafunzo |
| 7. | Bi. Mwanaidi M. Kalela | Mkaguzi Mkuu wa Ndani |
| 8. | Bw. Valency R. Kalunde | Mhasibu Mkuu |
| 9. | Bw. Bunyanzu J. Ntambi | Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano |
| 10. | Bi. Specioza Segesela | Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi |
| 11. | Bw.Hermes S. Rulagirwa | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA |
| 12. | Bw. Harry Mbogoro | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Sheria |

## 6. Mrajis wa Vyama vya Ushirika

Katika usimamizi wa kila siku wa Vyama vya Ushirika, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania huteua kwenye Serikali, mtu atakayefanya kazi katika Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwenye nafasi ya Mrajis wa Vyama vya Ushirika ambaye ndiye Msimamizi mkuu wa Vyama vya Ushirika Tanzania Bara. Aidha, Mrajis wa vyama vya Ushirika ndiye Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania Bara na ndiye msimamizi wa utekelezaji wa Sheria na Kanuni za Vyama vya Ushirika kwa ujumla.

## 7. Vipaumbele vya Tume

Katika kutekeleza majukumu yake, Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania chini ya Kamisheni inayoongozwa na Mwenyekiti wa KamisheniNdugu Abdulmajid Nsekela, imejiwekea vipaumbele vya kimkakati kwa ajili ya kufikia malengo yake kwa ufanisi zaidi. Vipaumbele hivyo ni kama ifuatavyo;

i. Uwekezaji katika mifumo ya kisasa ya kidijitali ili kuongeza ufanisi wa kiutendaji katika Vyama vya Ushirika, pamoja na Mamlaka za Usimamizi;

ii. Kuharakisha mchakato wa uanzishwaji wa Benki ya Taifa ya Ushirika ili kuviwezesha Vyama vya Ushirika kupata mikopo yenye riba nafuu;

iii. Kuhamasisha Mfumo wa Ushirika kujiendesha kibiashara wenye kuaminika na shindani ukijikita kwenye kuongeza thamani ya uzalishaji katika Vyama;

iv. Kuboresha Sera, Sheria na usimamizi wa ushirika ili kuchochea ukuaji na maendeleo ya Ushirika imara Tanzania;

v. Kuhamasisha Ushirika kwenye sekta mbalimbali na makundi maalum ili kuhakikisha wananchi wengi zaidi wananufaika na mfumo wa ushirika;

vi. Kuimarisha uwekezaji wa mali za ushirika katika uzalishaji; na

vii. Kushirikiana na wadau mbalimbali katika kutatua changamoto zilizopo kwenye ushirika.

## 8. OFISI ZA WARAJIS WASAIDIZI WA MIKOA NA MAWASILIANO YAO

1. Arusha
S.L.P 3050, Arusha
mrajis.arusha@ushirika.go.tz

2. Mtwara
S.L.P 235, Mtwara
mrajis.mtwara@ushirika.go.tz

3. Mwanza
S.L.P 119, Mwanza
mrajis.mwanza@ushirika.go.tz

4. Shinyanga
S.L.P 320, Shinyanga
mrajis.shinyanga@ushirika.go.tz

5. Kigoma
S.L.P 125, Kigoma
mrajis.kigoma@ushirika.go.tz

6. Simiyu
S.L.P 136, Bariadi
mrajis.simiyu@ushirika.go.tz

7. Tanga
S.L.P 3070, Tanga
mrajis.tanga@ushirika.go.tz

8. Njombe
S.L.P 1054, Njombe
mrajis.njombe@ushirika.go.tz

9. Dodoma
S.L.P 1054, Dodoma
mrajis.dodoma@ushirika.go.tz

10. Kilimanjaro S.L.P 3070, Moshi
mrajis.kilimanjaro@ushirika.go.tz

11. Mara
S.L.P 299, Musoma
mrajis.mara@ushirika.go.tz

12. Manyara
S.L.P 310, Babati
mrajis.manyara@ushirika.go,tz

13. Pwani
S.L.P 3080, Kibaha
mrajis.pwani@ushirika.go.tz

14. Ruvuma
S.L.P 74, Songea
mrajis.ruvuma@ushirika.go.tz

15. Tabora
S.L.P 315, Tabora
mrajis.tabora@ushirika.go.tz

16. Mbeya
S.L.P 754, Mbeya
mrajis.Mbeya@ushirika.go.tz

17. Songwe S.L.P 23, Mbozi
mrajis.songwe@ushirika.go.tz

18. Geita
S.L.P 1054 Geita
mrajis.geita@ushirika.go.tz

19. Kagera
S.L.P 299, Bukoba
mrajis.kagera@ushirika.go.tz

20. Dar es Salaam
S.L.P 5429, Dar es Salaam
mrajis.dar es salaam@ushirika.go.tz

21. Iringa
S.L.P 858, Iringa
mrajis.iringa@ushirika.go.tz

22. Singida S.L.P 5, Singida
mrajis.singida@ushirika.go.tz

23. Rukwa
S.L.P 128, Sumbawanga
mrajis.katavi@ushirika.go.tz

24. Lindi
S.L.P 668, Lindi
mrajis.lindi@ushirika.go.tz

25. Morogoro
S.L.P 650, Morogoro
mrajis.morogoro@ushirika.go.tz

26. Katavi
S.L.P 544, Mpanda
mrajis.katavi@ushirika.go.tz